
# Alasiri Online

www.ippmedia.com

ISSN 0856 Na. 001 Jumanne Aprili 16, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# ASLAY LIVE PASAKA

## Darassa aruka kubwiya unga



# BODI YA FILAMU KUFUNDA

Na Anaeli Mbise


BODI ya filamu Tanzania imeandaa kongamano litakalowajumuisha waigizaji, watayarishaji na wadau kwa lengo la kuwajengea uwezo katika sekta ya hiyo ili kujitambua, kujithathmini na kujitangaza.

Akizungumza na Alasiri Online, katibu mtendaji wa bodi ya filamu, Joyce Fissoo, amesema kongamano hilo litafanyika wiki hii katika ukumbi wa Suma JKT Mwenge.

"Kongamano hili litaanza saa 2 asubuhi hadi 12 jioni na kuwakutanisha wadau wote wa maigizo, watayarishaji na viongozi wa kidini ili kusaidia umuhimu wa msanii kujua haki zake na pia mikataba," amesema Fissoo.

Aidha amesema mada watakazozizungumzia ni kuhusiana na namna bora ya kujitangaza na pia kumfundisha msanii nidhamu ya kutumia fedha wakati anapozitapa.

"Wasanii wanapata fedha nyingi kutokana na kazi yao, lakini hawana nidhamu ya fedha na huenda ndiyo maana utakuta msanii anashindwa kumiliki hata nyumba," amesema Fissoo.



# ASLAY LIVE PASAKA

Na Anaeli Mbise


KWA mara ya kwanza tangu atoke Yamoto Band, staa wa muziki wa Bongo fleva, Aslay Isihaka amesema kuwa atafanya show Sikukuu ya Pasaka ndani ya Dar Live na bendi mpya.

Akizungumza na Alasiri Online, Aslay amesema kuwa, zipo zawadi nyingi amewatayarishia mashabiki hivyo wajitokeze kwa wingi kujionea.

"Mashabiki wote mnajua linapokuja suala la show huwa sirembi, nitakamua live kwa kutumia vyombo hakuna cha playback mwanzo mwisho ni burudani tu," amesema Aslay.

Naye Meneja wa Dar Live, Rajabu Mteta 'KP Mjomba' amesema kwa mara ya kwanza tangu Aslay afanye muziki kivyake hajawahi kushuka katika uwanja huo wa burudani.

"Siyo Dar Live tu, Aslay hajawahi kufanya show yoyote si Temeke wala Mbagala, kwa hiyo kwa mara ya kwanza atashuka Dar Live Pasaka hii na kuporomosha vibao vyake kibao kuanzia Hauna, Natamba, Totoa, Nibebe, Likizo," amesema KP Mjomba.



# DIANA SUGU WA MASIMANGO

Na Anaeli Mbise

MUIGIZAJI wa filamu za Kibongo, Diana Kimari amefunguka kuwa siku zote habadiliki kutokana na masimango ya watu yaliyojaa uongo.

Akizungumza na Alasiri Online, Diana amesema kuwa watu wanajisahau mno na kufikiri kuwa ukimsema mtu kwa maneno makali na kashfa kama siyo za kweli yatambadilisha.

"Niwakumbushe watu tu kuwa mimi ni yule yule, sibadiliki hata kidogo na maneno hayanifanyi kuwa Diana wa tofauti yaani haiwezi kutokea, naendelea na mambo yangu kama kawaida," amesema Diana.

Hivi karibuni Diana alidaiwa kupewa kichapo na mama wa mwigizaji Wema Sepetu, baada ya kudai hafurahishwi na tabia za mrembo huyo za kuropoka mambo ya watu.

# MAKUBWA YA FAIZA



**Na Anaeli Mbise**

MSANII wa filamu mwenye vituko lukuki Faiza Ally amefunguka kuwa hakuna kitu anachokipenda kama kufanya mapenzi.

Akizungumza na Alasiri Online, Faiza amesema kwamba kwa umri ambao anao sasa hivi kitu ambacho anakipenda ndiyo hicho, lakini kwa mwanaume msafi.

"Kwa nini nifiche jamani hobby yangu napenda sana kufanya mapenzi tena kwa umri nilionao ndiyo nafurahia zaidi na pia ili ni-enjoy zaidi ni kwa mwanaume msafi," amesema Faiza.

Miaka minne nyuma msanii huyo alikuwa mzazi mwenza na Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi maarufu kama 'Sugu' kabla ya kuachana.



# Mahaba ya Ray, Chuchu sarakasi

**Na Mary Kadoke**

MZAZI mwenza na muigizaji Ray the Greatest, Chuchu Hans amesema habari za kuachana na Ray, anazisikia kwenye redio mbao kama wengine, aidha amesema watasheherekea miaka kumi ya mahusiano yao mwezi ujao.

Amesema hayo alipofanya mahojiano na Alasiri Online akisisitiza kutokuwa na muda wa kusikia ya wazushi kwani athari zake ni baadhi ya mambo kusimama.

"Mimi na Ray ikifika mwezi wa tano tutatimiza miaka kumi kwenye mahusiano, hayo mengine siyajui," amesema.

"Hizo video hata mimi niliziona kama watu wengine niliumia kama binadamu, lakini nitafanyaje?" amesema.

Kumekuwa na video fupi kwenye mitandao ya kijamii ikimuonyesha Ray akiwa na mwanamke mmoja ambaye inadaiwa kuwa na mahusiano ya kimapenzi kwa sasa.

"Sijamuuliza kitu chochote kwa sababu nina mambo mengi ya kufanya unajua kufuatilia mambo ya mapenzi sometimes yanacost," amesema.

Ray na Chuchu wamebahatika kupata mtoto moja wa kiume Jaden (1).



# Darassa aruka kubwiya unga

**Na Mary Kadoke**

**MFOKAJI Darassa amekana matumizi ya madawa ya kulevya akifafanua kuwa anajua dhamira ya mtu aliyesambaza habari hizo hapo awali iliyokuwa kuzima ramani ya muziki wake.**

**Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akisisitiza kuwa hajawahi kutumia madawa hayo.**

**Hakuna kitu kama hicho sijawahi kutumia madawa ya kulevya namjua aliyesambaza habari hizo ila siwezi kumtaja, amesema.**

**Nia yake ilikuwa kunizima kimziki, lakini namshukuru Mungu nipo na naendelea kutoa hits, amesema**

**Habari za mfokaji huyu kutumia madawa ya kulevya zilizuka mwaka jana zikieleza mashabiki kutotarajia burudani yoyote kutoka kwake kwani tayari madawa hayo yalikuwa yameharibu ramani yake ya muziki.**

**Hata hivyo, tetesi hizo zilizimwa na kibao chake kipya alichokiachia baadaye kikiwa na jina la Tofauti chenye watazamaji 204,000 katika mtandao wa YouTube. Ngoma yake nyingine aliyowahi kutamba nayo ni Muziki yenye watazamaji Milioni 13.**